

# Maswali

1. Mbona Danieli alikuwa Babeli?
2. Mfalme wa Uajemi alikuwa nani kwa habari hii?
3. Mbona mawaziri hawakumpenda Danieli?
4. Mtego uliowekwa na mawaziri ulikuwa nini?
5. Danieli alifanya nini, na mara ngapi?
6. Nini ilifanyika kwa Danieli na mfalme alifanya nini ?
7. Mfalme alifanya nini asubuhi?
8. Nani alimtembelea Danieli?
9. Nini ilitendeka kwa simba?
10. Mfalme alifanya nini Danieli alipokuwa salama salamini?

# Majibu

1. Danieli alikuwa Babeli kwa sababu alichukuliwa matekwa huko.
2. Mfalme wa Uajemi alikuwa Dario.
3. Mawaziri hawakumpenda Danieli kwa sababu alipendwa na mfalme.
4. Mtego ulikuwa kutengeneza sheria mpya.
5. Danieli alimuomba Mungu wake mara tatu kwa siku.
6. Danieli alitupwa kwa shimo la simba na mfalme alijaribu kumuokoa.
7. Asubuhi mapema mfalme alikimbia kwa shimo kumuona Danieli.
8. Malaika alimtembelea Danieli.
9. Midomo ya simba ilifungwa.
10. Mfalme alipojua kwamba Danieli hajaumizwa, alituma barua yakutaka watu wote waabudu Mungu wa Danieli.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM



**Awamu ya 1 Mwaka wa 1**

## 31 Danieli na simba

### Marejeo

Danieli 6

### Kiini cha somo

Kuonyesha vile inatupasa tumwamini Mungu na kumuomba kila siku.

### Maneno maalum

1. Watu wasio wa kawaida [Wakipekee] + kutosikiliza + Wakaldayo + mfungwa + Danieli.
2. Danieli mzee + Waajemi + Dario + hekima + Mungu anasaidia + Mawaziri + mfungwa mgeni.
3. Mtego + sheria mpya + shimo la simba.
4. Mara 3 + maombi + Mawaziri wanakesha.
5. Mfalme asikitika + sheria haibadilishwi + okoa + tupia Simba.
6. Hakuna usingizi + asubuhi + jibu + Malaika + okoa + hakuumizwa.
7. Mfalme afurahi + barua + abudu Mungu.

31.1 Mungu alichagua taifa la Israeli kuwa la watu wake wakipekee. Aliwaahidi kwamba kila kitu kitaenda sawa ikiwa watampenda na wasikilize yote awaambiayo. Lakini Waisraeli hawakusikia kwa sababu hawa watu wa Mungu walinikataa. Walishambuliwa na taifa kali la Wakaldayo. Wengine wao walipelekwa Babeli kama wafungwa. Mmoja wawaliochukuliwa, alikuwa Danieli. Maisha yake ilyobaki aliihi Babeli.

31.2 Danieli alipokuwa mzee, Babeli ilipinduliwa na Waajemi na kutawaliwa na mfalme mpya. Huyo mfalme alikuwa Dario na alijua kwamba Danieli ana hekima. Mfalme alipokuwa na shida kubwa alimuuta Danieli. Danieli alijibu maswali yote kwa sababu alikuwa akimhusisha Mungu. Lakini mawaziri wenzake hawakumpenda Danieli kwa ajili mfalme alimuuta kila wakati. Danieli alikuwa mfugwa mgeni na hao walikuwa wakuu wa Babeli.

31.3 Mawaziri walimwekeea Danieli mtego. Walimwambia Dario aweke sheria mpya. Hiyo sheria ililazimisha watu wote wasiabudu Mungu au mtu yejote ila mfalme pekee kwa muda wa siku 30.

Atakayekataa kutii angetupwa ndani ya shimo ambamo simba waliishi. Hii sheria ilifanya mfalme akainuka na akakubaliana na hao mawaziri.

31.4 Danieli alifunga dirisha lake na kuomba Mungu mara tatu kwa siku. Sheria haikukubaliana na hayo kwa sababu Mungu alikuwa wa maana kwa Danieli kuliko sheria. Alijua atatupwa katika shimo la simba, lakini aliendelea kufungua dirisha na kuomba. Mawaziri walikesha wakamwona akiomba na wakaenda kumwambia Dario.



31.5 Mfalme aliposikia yaliyompata Danieli, alisikitika kwa kuiweka hiyo sheria. Alijaribu juu chini kumuokoa Daniel asitupwe ndani ya shimo la simba lakini sheria hangeweza kubadilishwa. Aliita Danieli na kumwambia kwamba Mungu unayemwabudu atakuokoa kutoka kwa simba. Watu hao walimchukuwa Danieli na kumtupa ndani ya shimo la simba.



31.6 Usiku huo mfalme hakulala wala hakula. Alitarajia Mungu wa Danieli atamwokoa. Asubuhi na mapema alitoka kwa nyumba ya kifalme na kukimbilia kwa shimo. Alipofika huko aliita Danieli kwa sauti, "Mungu wako amekuokoa?" Hakutarajia Danieli kuitika, lakini Danieli aliitika akajibu, "Mungu alinitumia malaika wake wakafunga midomo ya simba kwa sababu alijuwa mimi sijafanya makosa." Mfalme alifurahi na kuamrisha watumishi wake wamvute kutoka kwa shimo. Hakukuwa ameumizwa.

31.7 Mfalme alituma barua kwa watu wa ufalme wake wote. Aliwaambia juu ya Mungu wa Danieli. Aliwaambia vile Mungu alimuokoa Danieli kutoka kwa simba. Aliwambia kwamba wanatakiwa waabudu Mungu mkuu wa Danieli kwa sababu ni Mungu aliye hai. Inatupasa tuwe kama Danieli. Inatupasa tumuombe Mungu kila siku. Inatupasa tumuamini kila wakati. Tukimwamini atatuokoa kutoka kwa shida zetu.